



# MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



## HUDUMA YA MAJI SAFI NA SALAMA

### UBORA WA MAJI YANAYOSAMBAZWA

Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi ni Taasisi pekee inayotoa Huduma Bora ya Maji Safi na Salama katika Manispaa ya Moshi, Mji wa Mlima Kilimanjaro.




Mamlaka inasambaza Maji Safi na Salama kwa Wateja wake na Wakazi wote wa Moshi yanayotosheleza mahitaji yote ya Majumbani, Sehemu za Biashara na Viwandani katika kipindi cha **Muda** wote wa Saa Ishirini na Nne (24), huduma inayotosheleza mahitaji kwa matumizi ya kunywa, kuoshea, kupikia, usafi, mitambo ya viwandani, kumwagilia bustani na kuoshea magari (*lakini sio kwa kutumia mpira wa kwamwagilia*) na matumizi mengineyo.

Maji yanayosambazwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi hufuata Viwango vilivyowekwa Kitaifa na Kimataifa na:

- Serikali (Tanzania Temporary Standards) pamoja na
- Shirika la Afya Duniani (W.H.O Standards).

Kiwango cha ubora wa maji yanayosambazwa huzingatia ubora wa maji kikemikali na vimelea vinavyosababisha magonjwa

pamoja na ubora wa maji katika rangi, harufu na ladha. Kwa kawaida kuna viwango maalum vilivyowekwa na Serikali pamoja na Shirika la Afya Duniani ambavyo Mamlaka hulazimika kuvifikia kabla ya kusambaza maji kwa watumiaji.



Kwa kuzingatia jukumu la kusambaza maji katika viwango vilivyowekwa Kitaifa na Kimataifa, Mamlaka imelazimika kuweka **Mitambo ya Kusafisha na Kuongeza Ubora wa Maji** katika:

- **Vyanzo vya Maji vya Chemchem za Nsere na Shiri,**
- **Matanki ya Kuhifadhia Maji ya Kilimanjaro na Petershoff.**

Mamlaka inaamini faida ya mitambo hii inajionesha wazi kwa watumiaji wa maji hasa katika:

- **Kupunguza Matumizi ya Sabuni,**
- **Kupunguza kasi ya Magonjwa ya Tumbo, Kuhara damu, Kipindupindu na kadhalika,**
- **Kusaidia katika Kuhifadhi Fedha kwa matumizi mengine ya msingi ya familia.**

Ni wazi kwamba **Faida hizi huhalalisha matumizi ya maji safi** kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi na Gharama zake ambazo Wateja hulazimika kulipia.

***Lipia Ankara Yako ya Kila Mwezi ili Kujihakikishia Ubora wa Maji Unayoyatumia!***

**MKURUGENZI MTENDAJI  
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA  
MJINI MOSHI**

**S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164  
Barua Pepe: muwasa@kilionline.com**